
ENEO LA HABARİ

## SEHEMU YA 3

# Uchunguzi wa takataka

Sasa utachunguza takakata za aina nne muhimu: 1) plastiki 2) metali 3) karatasi na 4) gilasi. Tafuta wapi zinatoka, matatizo gani yanaweza kusababisha na vipi unaweza kudhibiti takataka hizo.

## 1 Plastiki




Neno plastsiki limetokana na neno la kigiriki Plastilcos maana yake –uwezo wa kusarifika. Tabia hii inazifanya plastiki kuwa maridhawa kwa utengenezaji wa vitu kama chupa, bandia za kuchezea watoto na vivurushi.

**Vipi plasitiki zinatengenezwa?** Plastiki zinatengenezwa kutokana na mafuta ghafi ya 'petroleum'. Kiasi asilimia nne (4%) ya mafuta yanayochimbwa duniani yanatumika kwa kuzalisha plastiki zote tunazozitumia katika maisha yetu ya kila siku. (Nusu inatumika katika usafirishaji na nusu kwa uzalishaji).

**Tatizo la plastiki.** Plastiki ni kitu kisichooza na kinakaa katika mazingira kwa muda mrefu sana. Sehemu zote ulimwenguni zinazofukiwa na kuchomwa takataka za plastiki ni mbaya kwa sababu ya kutolewa vitu vya hatari. Ijapokuwa hutoathirika, madhara yake yanajitokeza baada ya muda mrefu ambapo athari za kiafya zinaweza kuwa mbaya zaidi! Pia na wanyama wanaathirika. Kiasi cha ndege wa baharini milioni mbili wanakufa kila mwaka kwa kula au kuzongwa na plastiki.



(© Ulli Kloiber)

**Suluhisho kwa Zanzibar**

- Punguza matumizi ya vifurushi vya plastiki ikibidi; usinunue maji katika chupa za plastiki ikiwa unaweza kunywa gilasini ukiwa nyumbani. Nunua soda za chupa za kigae zinazorejeshwa dukani kuliko chupa za plastiki.
- Tutumia tena vitu vya plastiki badala ya kununua vipya.
- Sarifu: tenganisha chupa za plastiki kutoka kwenye takataka nyengine na zipeleke/ziuze katika sehemu zinazosarifiwa hapa Zanzibar. (Kwa maelezo zaidi ya mradi waone 'fanya mabadiliko')

*Kusarifu tena chupa moja ya plastiki inanusuru nguvu za kuwashia taa ya umeme ya wati 60 kwa masaa 6.*



**Mifuko ya plastiki: Uoni wa dunia**

Tokea mwaka1957 mifuko ya plastiki ilipoanza kutumika kwa mara ya kwanza huko Amerika ya kaskazini, makisio ya mifuko ya plastiki billion 500 hadi trilioni moja ya mifuko hiyo hutumika duniani kote. Hivyo mifuko ya plastiki zaidi ya milioni moja hutumika kwa dakika moja!!! Kutoka na kuzalishwa kwa mifuko mingi ya plastiki ni muhimu kuelewa athari iliyonayo mifuko hiyo kwa mazingira. Mfuko wa plastiki unapotupwa unaweza kuchukua mpaka miaka 1000 kuchakaa na kuharibika lakini kwa kweli hakuna anaejua kwasababu hapo zamani plastiki ilikuwa haipo.

**Zanzibar ni tofauti!!!**

Mwaka 2006, Zanzibar imepiga marufuku mifuko ya plastiki. Sheria inasema mtu yeyote atakae zalisha, atkae ingiza au atakae tumia mifuko ya plastiki atakabiliwa na adhabu ya kulipa faini hadi ya shilingi milioni moja au zaidi na hukumu ya kifungo cha hadi mwaka mmoja. Hata hivyo utumiaji wa sheria umekuwa na changamoto kubwa, Zanzibar.imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika uondoshaji wa mifuko ya plastiki kutoka visiwa vya unguja na Pemba. Hayo ni mafanikio ya kujivunia!




(© www.dailynews.co.tz)

## 2 Metali

Metali zinatumiwa sana kwa sababu ya sifa zake tofauti: ni madhubuti, hupitisha joto na umeme. Kuna aina 70 za metali, kati ya hizo chuma, chuma cha pua (chuma kizito) na aluminium zote ni muhimu zaidi.

**Metali zinatokea vipi?** Metali ni nadra kutokea katika hali safi (mfano dhahabu na fedha) kwa kawaida zinatokea kama mchanganyiko wa madini kama vile alluminium axide (bauxite).

**Tatizo.** Kutengeneza metali kwa kutumia maadini kunahitaji nishati za kutosha na baadhi ya metali zinaweza kuharibu mazingira yetu.

<u>**Suluhisho katika Zanzibar**</u>


- **Kupunguza matumizi:** tumia chupa za soda zinazorejeshwa kuliko kununua kinywaji cha soda ya kibati.
- **Kurejea matumizi:** (1) Tengeneza poti ya mmea kutoka kibati kikukuu (2) Kusanya vifuniko vya soda, fanya kazi za sanaa.
- **Kusarifu tena:** tenganisha metali kutoka kwenye taka nyengine, wasiliana na wahusika wa kusarifu tena katika Zanzibar na uza au changia mabaki ya metali.



(© www.guamsolidwastereceiver.org)

## 3 Karatasi

Karatasi ni moja iliyozoeleka zaidi katika matumizi ya kila siku. Kwa miaka mingi karatasi zilitengenezwa kwa mkono na kwa hivyo ilikuwa ghali. Watu walizitumia karatasi kwa uangalifu, na mara kwa mara walizihifadhi baada ya matumizi.



**Vipi karatasi inatengenezwa kwa miti?** Karatasi hutengenezwa kwa mbao za miti.

**Tatizo:** Ikiwa karatasi hazitosarifiwa tena (recycled) zitamalizia majaani na kuchomwa. Kwa kuongezea, ni uharibifu mkubwa ikiwa miti ya kutengenezea karatasi inavunwa kutoka msitu mkongwe.

**Suluhisho kwa Zanzibar**

- Kupunguza idadi ya karatasi
- Kurejea matumizi hasa mashuleni na kwenye makampuni.
- Kusarifu tena karatasi majumbani na mashuleni

## 4 Gilasi

Kwa mapana gilasi zilitumika kwa kuhifadhi vitu hasa kabla ya kuingizwa kwa plastiki.Soda nyingi za Zanzibar zililetwa ndani ya chupa za gilasi ambazo zilitakiwa zirejeshwe.

**Vipi gilasi zinatengenezwa?** Gilasi zinatengenezwa kutokana na mchanga na kemikali mbili za unga unga zinazojulikana kuwa ni soda na chokaa. Katika kiwanda cha gilasi, mchanganyiko wa vitu vinavyotengenezewa gilasi huunguzwa kwa nyuzi joto kubwa mpaka mchanganyiko unakuwa maji mazito ambayo yanaweza yakasarifiwa kuwa vitu vingi vyenyematumizi. Kwa mfano chupa, gilasi za kunywea maji na matungi ya taa.

**Tatizo:** uzalishaji wa gilasi unatumia nishati nyingi sana. Ikiwa gilasi itazikwa haitovunjika na itakaa kwa mamilion ya miaka katika hali hiyo. Gilasi iliyovunjika inakuwa na ncha kali na huleta madhara kwa wanadamu na wanyama.



(© www.guamsolidwastereceiver.org)

**Suluhisho kwa Zanzibar**

- Punguza uzalishaji wa vitu vya gilasi
- Tutumia tena chupa na majagi kwa kutilia jamu, juisi au maji. Kuwa mbunifu fanya matumizi mengine kutokana na chupa za vigae, mfano kwa kufanya vitu vilivyopambwa kwa vipande vya vigae au mawe ya rangi au kufanya kengele za upepo.
- Rejea matumizi kwa vigae kunafanyika ulimwengu mzima. Kwa Zanzibar inawezekana kurejesha chupa za soda za vigae madukani hata hvyo chupa za mvinyo na bia bado hazijakusanywa na kusanifiwa.

